

Elimu Juu ya Pepo

Milki ya Kimwili

 ...msaada wa Bwana, tungeweza kuendeleza mkutano moja kwa moja, sisi wenyewe. Hiyo ndiyo sababu ninafurahi kuuona ukipita kidogo, kwa sababu hiyo moja. Ninaamini Bwana atatusaidia kufanya jambo hilo. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, mnajua kuna-...

Ninawapenda mameneja wangu. Nina ndugu wazuri sana, Bosworth, Baxter, Lindsay, Moore, wote, nina watano, Baron Von Blomberg. Wao ni watu wazuri tu sana. Lakini kuna kitu fulani tu kuhusu, unapokusanya kundi la watu pamoja, mmoja ana jambo moja, mwingine ana lingine. Wakati mwingine huwa kinyume na yale ninayowazia mwenyewe. Kwa hiyo ni—ni—ninajisikia kama niko huru tu sasa. Tunaweza tu kuwa na wakati wa furaha, tukunje mikono ya mashati yetu, tupige mbizi na kula. Ninafikiria juu ya kukunja mikono ya shati lako na kuwa na wa—wakati mzuri.

Biblia yangu ya kwanza ilikuwa maumbile. Nilijifunza habari za Mungu katika maumbile. Nami ninapenda kuvua samaki. Jinsi ninavyopenda kuvua samaki! Nawe unapenda kuvua samaki, kadogoo? Kama unapenda kuvua samaki, na unampenda mama yako, utakuwa mvulana mzuri. Na hata wongofu wangu hakuondoa jambo hilo kabisa ndani yangu. Kwa hiyo siku moja nilikuwa huko juu milimani, nikivua samaki. Sasa, jambo hili ni kwa manufaa tu ya mvulana huyu mdogo. Nami nilikuwa ninavua samaki kule juu milimani...Na kwa ajili ya hao watoto wengine wadogo, bila shaka, wanaoketi hapa. Nami nilikuwa nikivua samaki wa mtoni. Na, loo, ni ajabu, kwenye msimu wa kuchanua majani. Ninaendelea namna hiyo, na kulikuwa na samaki wa mtoni kwenye shimo hilo lingine, mwajua, namna hiyo. Nilikuwa tu nikimsifu Bwana na kuwa na wakati mzuri sana, kupaza sauti. Mara kwa mara, niliweka chini uzi wangu wa kuvulia. Ninaamini katika kupiga shangwe. Amina. Kweli ninaamini. Maana, ninajua jambo fulani hunishika. Na... [Sehemu tupu kwenye kanda.]

² Kuna madubu wengi sana kwenye nchi ile kule juu, huko New Hampshire. Nina kambi ndogo kule juu, ambako ninavua samaki. Nilikuwa na maskini hema dogo kuukuu lililokuwa kule, hema kuukuu la watu wawili nilimokuwa ninaishi. Na dubu mweusi ndiye kitu chenye utundu sana kilichopo. Kwa hiyo, maskini mama dubu na watoto wake kadha walikuwa wameingia mle, na hapo wakaharibu sana hema yangu!

³ Sasa, unafikiri nilipaswa kumfanyia nini huyo dubu, ewe msichana mdogo huko nyuma mwenye nywele nyekundu, huko nyuma? Nilipaswa kumfukuza kabisa, sivyo?

⁴ Lakini mambo aliyofanya ni haya. Aliingia, akararua hema langu na kuvuruga kila kitu, na kula chakula changu chote nilichokuwa nacho pale, naye alikuwa tu akijifurahisha. Kwa hiyo nilipokuja, huyoo akatoroka. Kisha akawaita watoto wake, na kitoto kimoja kikamkimbilia. Na huyo mwingine hata hakukimbia; aliketi tu pale. Alikuwa ameelekeza mgongo wake kwangu, namna *hii*, naye alikuwa anafanya kitu fulani. Nami sikuwa na kitu cho chote mkononi mwangu ila shoka la kale la mkono. Nilikuwa nikichanja miti michache ya mielda mifupi kule chini. Vema, akakimbia umbali kama wa, loo, nafikiri wa ule mti wa simu kule nje, kisha akakaa. Akakiita maskini kitoto chake kidogo nacho hakikumjali. Aliendelea tu kukaa pale.

⁵ Nikafikiri, “Maskini jamaa yule mdogo anafanya nini?” Nikasonga karibu zaidi. Niliogopa kumkaribia sana, nikiogopa atanipiga kucha. Basi—basi si—sikuweza kuona mti, nami najua yeye angeweza kupanda pia. Kwa hiyo, wala sikutaka kumkaribia sana, maana ninajua tabia ya dubu. Kwa hiyo nikasogea karibu kidogo. Na mnajua kilichotukia?

⁶ Sasa, mimi ninapenda mikate ya kumimina. Ni wangapi wenu ninyi vijana mnapenda mikate ya kumimina? Loo, jamani! Loo, mimi. . . Vijana wakubwa pia. Niliwaona wakiinua mikono yao pia. Sote tunapenda mikate ya kumimina, nami naipenda tu, nami napenda kuimimina asali. Nikiwa Mbatisti, wajua, hilo ndilo linalotufanya tudumu wanyofu, wajua, ni asali, wajua. Kwa hiyo, na sikiliza, mimi siinyunyizii, ninaibatiza hasa. Ninaimiminia kweli mpaka imeenea vizuri na kuwa nzito. Mimi siinyunyizii kidogo tu hapa na pale. Ninaimwagia kweli kweli, ninaijaza yote kwa asali.

⁷ Na basi, unajua, nilikuwa na ndoo ya asali kule, nusu galoni ya ndoo ya asali. Na madubu wanapenda asali sana. Kwa hiyo maskini jamaa maskini jamaa huyu mdogo alikuwa ameingia kule na kufunua mfuniko wa ndoo ile ya asali, naye alikuwa ameketi pale namna *hii*, ameshika hii ndoo ndogo ya asali chini ya mkono wake, namna *hii*. Akachukua ninii. . . Hakujua namna ya kuila, kama ambavyo wewe ungeila, unajua, kwa hiyo yeye alichovya tu kiganja cha mkono wake mdogo ndani na kuilamba namna *hiyo*, na kuilamba. Kisha akageuka kuniangalia, na maskini macho yake mdogo yote yalikuwa yamezimba kwa asali, tumbo lake linameremeta sana liwezavyo kuwa, kwa asali. Alikuwa tu ameketi pale, akichovya mkono wake ndani na kulamba asali, namna *hiyo*, kwa bidii tu alivyoweza kunamba.

⁸ Loo, jamani, nilifikiria juu ya mkutano mzuri wa kikale wa Roho Mtakatifu, tunapoifungua ndoo tu, tunatumbukiza mkono

wetu chini kwenye gudulia na kulamba. Kuendelea tu, unajua, kulamba tu.

⁹ Na unajua jambo la kuchekeka lilikuwa ni nini, lakini? Baada ya jamaa huyo mdogo kupata kiasi alichoweza, aliiangusha ile ndoo chini akakimbia akatoka pale. Unajua yaliyotukia? Yule mama dubu na yule mtoto mwingine wa dubu wakaingilia kumlamba, ili kuitwaa ile asali.

¹⁰ Kwa hiyo, naam, labada mkutano wetu utakuwa kitu kama hicho, natumaini, ili tupate kuendelea kuwaambia wengine, na utukufu wa Mungu ukitushukia. Vema.

¹¹ ...Ninafurahi kuona ninyi watoto wadogo mmetoka. Ninapenda kuwaambia kitu kama hicho. Na labda kesho alasiri, tutakuwa na wakati mwingi zaidi, na—na tunaweza kuzungumza zaidi kidogo. Nasi tutazungumza na baba na mama sasa kuhusu jambo fulani.

¹² Tutazungumza juu ya *Elimu Juu ya Pepo*. Katika Zaburi 103:1 hadi 3, tunasoma aya hizi. Karibu kila mhudumu na kasisi, ama Msomaji wa Biblia, anazijua kwa moyo.

Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA: naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu.

Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, wala usizisahau fadhili zake zote:

Akusamehe maovu yako yote; akuponya magonjwa yako yote;

¹³ Ninawatakeni muone pale, ilikuwa ni “yote.” “Akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote.” Sasa tunaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

¹⁴ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunakushukuru alasiri ya leo, kwa kuwepo huku. Tunakushukuru kwa ajili ya watoto hawa wadogo wanaoketi hapa, wao ndio wanaume wa kesho, na wanawake, kama ikiwepo kesho, kama Yesu akikawia. Na sasa, Baba, tunaomba ya kwamba—ya kwamba utatubariki sasa kwa kuwa sasa tunazungumza juu ya Neno Lako, na juu ya adui mkubwa tuliye naye, Shetani. Tunaomba, Mungu, ya kwamba utaturuhusu tuweke mstari wa mbele wa vita, mtambo wa vita hapa, zile nguvu za Mungu, ambazo zitamkabili usiku wa leo katika kila inchi ya uwanja wake, Bwana, na kumwonyesha ya kwamba hana haki za kisheria hata kidogo, ya kwamba Kristo alimshinda badala yetu pale Kalvari, wakati alipokufa, naye akazivunjaa enzi na kumnyang’anya Shetani kila—kila nguvu aliyokuwa nayo. Na, Mungu, tupe hekima na ufahamu sasa, kujua na kuelezea watu jinsi ambavyo wangeweza kujua jinsi ya kuponywa na kumshinda Shetani. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

¹⁵ Sasa kwa dakika chache tutazungumza juu ya *Elimu Juu ya Pepo*. Mnasikia mambo mengi sana juu ya pepo. Sasa, kesho

alasiri labda tutamaliza. Nilitaka siku mbili za juma hili, hata hivyo, kuhubiri juu ya jambo hili, ninii tu . . . ama siku mbili kwa ajili ya ibada za alasiri, kuzungumzia jambo hili.

¹⁶ Sasa, jambo la kwanza, kwamba pepo ni nini. Unawasikia watu wengi sana wakizungumzia juu ya pepo. Vema, sasa, “pepo, ibilisi,” yote yanatokana na neno moja, na katika Kiingereza huitwa “mtesi.” Jamaa anayetesa ni ibilisi, yule mwovu. Yeye anasema . . . Sasa, Biblia leo ni, kwa karibu watu wote, kwa watu wengi, ni kitabu cha kale cha nyuma ambacho babu na nyanya walisoma, ama kitu kama hicho. “Hakina lo lote, ni cha wazee, na kadhalika.” Lakini hilo ni kosa. Ni cha kila mtu. Na pepo ni watesi wanaotutesa.

¹⁷ Sasa, kuna pepo wanaoingia katika nafsi ya mwanadamu, na hiyo ni kusema, kimsamiati, hiyo ingekuwa—hiyo ingekuwa katika ninii . . . Ningesema jambo hili, hata hivyo, pepo anayeingia nafsini ni kitu ambacho kinaitesa nafsi.

¹⁸ Mara nyingi unaweza kumwona mtu ambaye labda ana kichaa. Sasa, wanaweza kuwa hata hivyo ni mtu aliyeongoka, amejazwa na Roho Mtakatifu, ha hata hivyo awe ni mwenda wazimu kabisa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hilo halina uhusiano wo wote na nafsi. Ni mtesi, unaona, kitu kinachowatesa.

¹⁹ Sasa, magonjwa yote, hatuna budi kutambua kwanza ya kwamba magonjwa yote yalitoka kwa Ibilisi. Mungu si mwanzilishi wa magonjwa. Hakuna magonjwa yanayotoka kwa Mungu. Mungu mara kwa mara anaruhusu Shetani akupe ugonjwa ndani yako, kama mjeledi wa kukurudisha kwenye nyumba ya Mungu, ulipokaidi. Lakini magonjwa, chanzo chake, yatokana na Ibilisi. Ungeweza kuwazia mtu angeamini ya kwamba Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, angekuwa mwanzilishi wa kitu kama magonjwa na mauti? Vema, la, si Yeye, kamwe hajawa hivyo, hatakuwa hivyo kamwe. Mungu huruhusu mauti kwa sababu ya ukaidi. Mungu huruhusu mauti. Kama alivyosema mwandishi mmoja, “Yote ambayo mauti yanaweza kufanya, Mungu aliyafungia kwenye mkokoteni na inatuvuta na kutupeleka katika Uwepo wa Mungu, mwamini.” Lakini neno *mauti* linamaanisha “utengano.”

²⁰ Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kuwamwini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Kisha akasema, “Mimi ndimi ufufuo, Uzima, yeye aniaminiye Mimi, ijapokuwa amekufa, atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kabisa.” Nasi tunaweka miili yetu sisi kwa sisi kwenye kaburi letu lisilo na mtakatifu. “Lakini hatakufa kabisa.”

²¹ Sasa kama ukiangalia wakati aliponena habari za Lazaro, Yeye alisema, “Lazaro amelala.”

²² Wanafuzi, watu kama tulivyo sisi, wakasema, “Loo, ikiwa yeye analala atapona vema. Yeye alimaanisha kupumzika,” walivyodhani wao.

²³ Lakini yeye alikuja na kuzungumza nao katika lugha yao. Akasema, “Amekufa, vile mnavyoamini. Lakini,” kasema, “Ninaenda kumwamsha, kumwamsha.” Mnaona? Mnaona? Unapo-...

²⁴ *Mauti* maana yake ni “tenga.” Sasa, kama mmoja wenu akininii, mmoja wa familia yenu akifa, ama cho chote kile, ananinii, kama ameongoka, hawajakufa. Katika mawazo ya kibinadamu wao wamekufa. Lakini wao wametenganishwa tu nasi, lakini wako katika Uwepo wa Mungu. Hawakufa, wala hawawezi kufa, haiwezekani kwao kufa. Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani.” Kwa hiyo, hawezi kufa. Cho chote kisichopatikana na mauti, cha Milele, hakiwezi kuangamia. Ni Uzima usioharibika. Yeye anao Huo kwa sababu Mungu amempa Huo. Na si—si kwa kustahili kwake; ni kwa... Hauna masharti. Mungu amempa yeye Huo.

²⁵ Mungu ndiye aitaye. Hakuna mtu awezaye kuja kwa Mungu asipoitwa na Mungu. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipoitwa na Baba Yangu, asipovutwa.” Hiyo ni kweli? Kwa hiyo mambo yote ni Mungu. Labda kesho alasiri tutapata zaidi kidogo juu ya jambo hilo, maana ninataka kuweka wazi jambo hili la *magonjwa*, kwenu, ili mpate kuona jambo hilo.

²⁶ Kuna wakati ambapo tulianza uhai katika baba wa babu yetu. Mnajua jambo hilo. Daktari anajua jambo hilo. Vema, mnajua, pia, ninyi wasomaji wa Biblia. Unajua ile mbegu ya uhai ilianza ndani ya baba wa babu yako, ikawa mbegu hai, ikapitia kwa babu yako, halafu ikaingia kwa baba yako, halafu kwa mama yako na kufikia mahali ulipo sasa. Hiyo ni kweli. Maandiko hata yanafundisha jambo hilo. Haya hapa Maandiko kwa ajili yako kama ukitaka. Ninaamini ya kwamba yalisema ya kwamba Lawi alilipa zaka alipokuwa katika viuno vya Ibrahimu, ambaye alikuwa baba wa babu yake. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, mnaona, hiyo mbegu ya uhai ilianza kule nyuma.

²⁷ Lakini nafsi zenu zilifanywa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Mungu alipomuumba mwanadamu katika mfano Wake Mwenyewe; roho ya mtu; si mtu *fulani* katika mfano Wake Mwenyewe lakini *mtu* katika mfano Wake Mwenyewe. Mnaona? Naye akawafanya mwanamume na mwanamke, kabla Yeye hajakuwa na mwanadamu katika mavumbi ya nchi. Laiti tungalikuwa na nafasi alasiri ya leo, tuchukue wakati wa kutosha na kurudi nyuma tuingilie jambo hilo. Tuone tu jinsi Mungu... Sasa, liko katikati ya mstari, lakini, unapoliona, linaambatana na huo mstari. Mnaona? Jinsi ambavyo Mungu,

kule nyuma hapo mwanzo, alichotenda kule, na jinsi alivyoshuka chini akaingia duniani na jinsi alivyomfanya mtu katika mfano Wake; na ndipo Mungu akageuka na akafanyika katika mfano wa mwanadamu, apate kumkomboa mwanadamu.

²⁸ Sasa, wakati Mungu alipomfanya mtu katika mfano Wake, alikuwa mtu aliye roho. Na basi hapakuwepo na mtu wa kuilima ardhi. Ndipo akamuumba mtu kutoka katika mavumbi ya ardhi. Sasa, wachunguzi wa miaka, na kadhalika, na hawa watu wanaotafiti na kuchukua mifupa ya kale, na kadhalika, na kuamini katika mageuzi yanayoendelea. . . Ninaamini katika mageuzi ya kweli yanayoendelea. Mwanadamu alitokana na yeye mwenyewe, lakini si mwili mzima kutoka kwenye seli moja. La, bwana, kwa sababu nde—ndege amekuwa ndege tangu Mungu alipomuumba ndege, na tumbili amekuwa daima ni tumbili, mwanadamu amekuwa daima ni mwanadamu. Hiyo ni kweli.

²⁹ Sasa, nilikuwa nikizungumza na daktari fulani hapa muda kidogo uliopita, huko Louisville. Akasema, “Mbona, Kasisi Branham!” Nilikuwa nikizungumza jinsi ambavyo wananchi wa Afrika, jinsi wanavyokula, kushuka tu kwenye. . . Loo, baadhi ya vitu vya kutisha sana ungaliweza kuona, jinsi ambavyo wangekula! Wanaokota tu vitu vilivyooza, vyenye mabuu, wanavitikisa tu, mabuu na kila kitu. Hawajali. Unaona? Wao walisema. . . Wanakunywa cho chote kile, haijalishi ni kitu gani. Yeye akasema, “Lakini, Kasisi Branham, hao watu si wanadamu.”

Nikasema, “Loo, ndiyo, ni wanadamu. Wao hakika ni wanadamu.”

³⁰ Nikasema, “Kitu kilicho karibu sana na mwanadamu, katika tabaka ya wanyama, ni sokwe mtu. Nanyi mmejaribu kwa miaka elfu nne kupata tamshi moja kutoka kwa sokwe huyo, naye hawezi kufanya jambo hilo,” nikasema, “kwa maana hawezi kufikiri. Hana cha kufikiri nacho.” Loo, unaweza kumfunza mambo madogo madogo kama farasi, kwenda kulia na kushoto, ama kuvaa miwani, ama kuvuta msokoto, kukaa vizuri juu ya baiskeli, kupanda farasi, ama kitu kama hicho, lakini ni kama tu kwenda kulia na kushoto, kwa farasi, ama kwa mbwa ama kitu kama hicho.” Nikasema, “Yeye ni mnyama.”

³¹ “Lakini hebu wacha nirudi huko Afrika, kwenye kabila la nyuma sana walilo nalo, na hilo ni lile kabila dogo la mbilikimo.” Nami nikasema, “Labda babu wa babu wa babu wa babu yake hajawahi kuona mzungu wala cho chote kile. Jambo tu analojua, hata hajui ni upi mkono wake wa kulia ama wa kushoto. Jambo pekee analojua ni kula, naye hula cho chote anachoweza kupata, kama ni nyama ya mwanadamu, cho chote kile, yeye hajali, mradi tu anakula. Lakini hebu nimchukue kwenye umri wa miaka mitano, na atakapofikia umri wa miaka kumi na tano atazungumza Kiingereza kizuri na atakuwa na elimu nzuri. Kwa

nini? Yeye ana nafsi. Mungu alimfanya mwanadamu, naye ana haki ya kusikia Injili, angalau mara moja, kama tuliyo nayo ya kuhubiri mahali hapa, kila mahali Marekani, kwa watu, tena na tena, na kusihi, kushawishi na kila kitu. Hebu aisikie wakati mmoja, na umwangelie akipiga makelele na kukimbilia madhabahuni haraka sana.” Mnaona? Naam, bwana!

³² Hivyo ndivyo ulivyo moyo wangu, ndugu, leo, ninapowazia habari za Afrika, na maskini mikono hiyo myeusi imeinuliwa juu, wakisema, “Ndugu Branham, mara moja zaidi kuhusu Yesu!” Loo, rehema! Kuna kitu fulani ndani yangu kinachosukuma na kuwaka moto. Haraka tu nitakapopata pesa za kutosha, ninaenda huko, pia. Hivyo ndivyo ninavyofanya na kila senti ninayopata, kila kitu, Mungu anajua, mbali na zile ninazoweza kula. Na watu wengi sana hunipa nguo zangu za kuvaa. Na zile tu ninazoweza kutumia kupata riziki yangu tu, mimi mwenyewe, kwa uangalifu sana tu niwezavyo, ninaziingiza moja kwa moja kwenye mfuko wa fedha wa kimishenari ambao serikali imeandaa. Hata sizilipii kodi ya mapato. Nikiisha kukusanya dola elfu tatu ama nne, tano, huenda katika nchi za ng’ambo na kuwahubiria watu hao Injili ambapo ninajua ya kwamba kwenye hiyo siku nitawajibika kutoa hesabu. Nami nitajua nitakachowajibika.

³³ Nikuwa, nilipoingia kwenye mji fulani, ningefanya mkutano mkubwa zamani kule wakati walipokuwa na pesa nyingi, nao wanakuwa na mikutano mikubwa na maelfu ya dola, ningewapa Msalaba Mwekundu na kadhalika. Sasa, sasa, si kuwalaumu, lakini wao wanashuka barabarani na gari la dola elfu nne, lenye mapambo ya vinundu vya almasi, wakivuta msokoto, na mshahara wa dola mia tano kwa juma kwa pesa ambazo watu wagonjwa... La, bwana! Sivyo, kwa kweli! Na juu ya hizi, mara unapotoka kwenye mji huo, wao wanasema, “watakatifu wanaojifingirisha,” na kila kitu namna hiyo, na kukutania, na kuichukia dini tunayotetea. La, bwana!

³⁴ Ninazichukua mimi mwenyewe, na mbele ya Mungu kama Hakimu wangu, ninaziweka katika kazi ya Injili huko ng’ambo, ili kwamba nijue ya kwamba Siku ile ambayo nitaninii...wakati itakaponibidi kutoa hesabu ya uwakili wangu, zinatumiwa vizuri. Hiyo ni kweli kabisa, maana ninatambua vile ninavyowatendea watu ninamtendea Mungu. Vile msimamo wangu ulivyo kwenu ndio msimamo wangu kwa Kristo. Na msimamo wenu kwangu ni jambo lile lile, hiyo ni kweli, kwa Kristo.

³⁵ Sasa, kuona watu kama hao, na kuona jinsi ambavyo mwanadamu, basi, akiwa na nafsi isiyopatikana na mauti sasa, isiyoweza kufa, isiyoweza kuangamia, hawezi kufanya lo lote ila kuwa na Uzima wa Milele, ambao Mungu kwa ukuu, katika mapenzi Yake Mwenyewe, alikupa wewe. Na sasa, basi, sasa mimi... .

³⁶ Hebu nisahihishe jambo hili kidogo tu, ama niseme jambo fulani. Mtu fulani ataondoka na kusema, “Ndugu Branham ni Mkalvini.” La, sivyo nilivyo. Mimi ni Mkalvini mradi tu Ukalvini umo katika Biblia. Lakini hapo Ukalvini unapotoka nje ya Biblia, basi mimi ni Muarminia, mnaona. Ninaamini katika utakatifu na ninaamini katika Ukalvini, pia. Lakini, wote wawili, mmoja alikimbilia kwenye upande mmoja na kushika njia *hii* na mmoja alikimbilia upande ule akashika njia *ile*. Kama isingekuwa ni kwa ajili ya Kitabu cha Waefeso, kuturudisha na kutuweka mahali panapofaa ambapo Mungu alituweka, sote tungekuwa tumechanganyikiwa. Lakini wote wawili wana fundisho, lakini walikwamia hapo, kila mmoja, hao ni wale wa utakatifu na Wakalvini, pia, Waarminia. Sasa, Wakalvini wana kitu fulani kilicho cha kweli. Ninaamini hivyo, ya kwamba fundisho la Kalvini. . .

³⁷ Ninaamini hivi. Katika usalama, ninaamini Kanisa lina Usalama wa Milele. Msomaji ye yote wa Biblia anajua jambo hilo, maana Mungu tayari alisema lingetokea kule ng'ambo bila kunyanzi. Hiyo ni kweli? Basi, litakuweko. Hiyo ni kweli? Bi- . . . Kanisa limewekwa kwenye usalama Milele. Sasa, kwamba wewe umo ndani ya Kanisa, ndilo jambo la pili. Kama uko ndani ya hilo Kanisa, vema, umewekwa kwenye usalama pamoja na Kanisa, lakini afadhali udumu katika Kanisa. Na unainginaje katika Kanisa? Kwa kusalimiana kwa mikono? La. Kuweka jina lako katika kile kitabu? La, bwana. “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa katika Mwili mmoja.” Na Mwili huo, uliohukumiwa na Mungu pale Kalvari, ulikuwa ni Mwili wa Yesu Kristo, nasi tunabatizwa katika Mwili huo kwa Roho Mmoja. Tuna Usalama wa Milele mradi tu tumo katika Mwili wa Kristo, hakuna kinachoweza kututenganisha, hakuna kinachoweza kutugusa. Kama ukitoka, unatoka kwa hiari yako mwenyewe. Lakini kwa hakika tu, kama uko katika Mwili wa Kristo, kwa hakika kama Yesu alivyofufuka katika wafu, na utafufuka. Mungu tayari amekwisha kufanya jambo hilo. Yeye. . .

³⁸ Huwezi kutenda dhambi. Loo, unatenda. . . Ninaweza kuwa mwenye dhambi machoni pako, lakini kama niko katika Kristo, Mungu haoni jambo hilo, kwa sababu dhambi zake. . . Damu Yake inalipia dhambi zangu pale. Unaona? Siwezi kutenda dhambi. “Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu hawezi kutenda dhambi. Uzao wa Mungu hukaa ndani yake.” Mnaona? Yeye, yeye yuko tayari, kama akifanya makosa, hakika, mara moja yeye yuko tayari kutubu. Kama yeye ni Mkristo halisi, atafanya jambo hilo. Kama hataki kutubu, yeye anaonyesha hana cho chote, kwanza. Hiyo ni kweli. Hana lo lote, kwanza. Lakini kama yeye ni Mkristo halisi. . .

³⁹ Papa hapa, unapanda chembe ya ngano ardhini, daima itakuwa chembe ya ngano. Magugu yanaweza kuizunguka kila

mahali, na cho chote kile, lakini itakuwa chembe ya ngano maishani mwake mwote. Hiyo ni kweli? Na kama mtu kweli amezaliwa kwa Roho wa Mungu, yeye haingii na kutoka, na kurudi nyuma na kadhalika, na huyo kaenda zake ulimwenguni na atoke hapa nje. La, bwana. La, la. Wewe si gugu siku moja na chembe ya ngano kesho yake. Mungu hana hayo shambani. Naam, bwana. Kama umezaliwa kwa Roho wa Mungu, wewe ni Mkristo tangu wakati huo mpaka . . . mpaka utakapoondoka, halafu basi wewe u—unaishi milele, pamoja na Mungu. Hiyo ni kweli, kama uko katika lile Kanisa.

⁴⁰ Sasa, sasa hebu na tuzungumzie juu ya upande wa mauti. Sasa, mtu katika hali hiyo, katika hali kama hiyo, anawezaje kuwa mgonjwa? Kwa sababu mwili wako haujakombolewa bado. Mwili wako haujakombolewa. Haidhuru vipi, haidhuru wewe ni mzuri vipi, na ni mtauwa vipi, ni mtakatifu vipi, na una Roho Mtakatifu vipi, hiyo ni nafsi yako tu. Na nafsi yako haijakamilika bado. Ina ile Baraka tu, ile ahadi ya Mungu, ambayo ni arabuni ya wokovu wetu. Lakini sasa kama hatuna arabuni ya ufufuo wetu, hatuna uponyaji wa Kiungu, basi sitakuwa na hakika wala cho chote kile kunithibitishia ya kwamba kuna ufufuo.

⁴¹ Ni kama tu vile kama Kristo haishi moyoni mwangu, kama itanibidi kulichukua kutoka kwenye namna fulani ya—ya kitu cha kisaikolojia kule zamani za kale, inibidi kuamini mahali fulani kama hapo, vema, basi kidogo ni—ni—ningelitilia shaka. Na hiyo ndiyo sababu, huko Afrika, walipokuja, hapa walikuja wamishenari, wakiwaleta maelfu ya wenyeji wa huko, nao walikuwa wamebeba sanamu ndogo za udongo za kuabudu na cho chote kile, ni kwa sababu walikuwa wamesikia upande wa kiakili tu wa Biblia. Hiyo ni kweli. Na kanisa langu mwenyewe ni Batisti, Methodisti, Presbiteri, yote yaliyoenda kule. Lakini walipoona nguvu za Mungu zikija katika madhihirisho, hilo lilitosha, walijua basi ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu.

⁴² Lakini, sasa, ni kitu gani kinachoanzisha magonjwa haya? Sasa, jambo la kwanza, ni roho fulani kabla haijakuwa ugonjwa, kama tu vile wewe ulivyokuwa roho kabla hujakuwa mwanadamu. Sasa nitamchukua Ndugu Willett hapa kama mfano. Ndugu Willett, mimi. . . Kulikuwa na wakati ambapo mimi na wewe hatukuwa kitu. Na jambo la kwanza, Mungu akatupa uhai. Na hebu tuchukue, tuseme, kama nikiutenganisha mwili wako alasiri ya leo, wewe umetengenezwa kwa kundi la seli, zilizoshikamanishwa kwa atomi. Na sasa, siku moja hizo atomi zitaangamizwa, Yesu akikawia. Utarudi ulivyokuwa mwanzo. Zitakuwa tu kama zilivyokuwa hapo mwanzo, zitarudi hewani. Lakini wakati roho yako itakaporudi, hizo atomi zitakusanyika pamoja tena pamoja na roho hii na kumleta Ndugu Willett mwingine kama tu yule yule, ila tu ni kijana zaidi, wakati alipokuwa katika upeo wa ujana wake.

⁴³ Mtu anapopitisha umri wa miaka ishirini na mitano, anapata makunyanzi machache chini ya macho yake, na mvi chache zinazoanza kuingia. Itakuwa hivyo, kwa maana mauti inakutafuta. Na moja ya siku hizi itakuchukua. Haidhuru wewe ni nani, itakuchukua. Lakini hatimaye... Utafikia kwenye kona hapa, na Mungu atakutoa kwenye kona hiyo, kisha utaingia katika kona hii *hapa*, na mauti karibu itakupata, na mahali hapa, lakini baada ya kitambo kidogo itakupata. Lakini basi, kile mauti yanachoweza kufanya, yanasababisha madhara mengi, halafu basi kwenye... wakati imefanya yote inachoweza kufanya... Wakati Mungu alipokupa uhai huu, nawe ulikuwa katika upeo wa ujana wako, kwenye kama umri wa miaka ishirini na mitatu, wakati utakapokuja kwenye ule ufufuo utarudi tu vile vile kabisa kama ulivyokuwa ulipokuwa na umri wa miaka ishirini na mitatu, ishirini na mitano, kabla mauti haijaingia. Mauti itafanya cho chote inachoweza kufanya. Itaingia mle, lakini wewe utarudi moja kwa moja jinsi ulivyokuwa.

⁴⁴ Sasa, kama kila moja ya—ya seli zako mwilini mwako, hebu na tuzitenganishe sasa, unatenganisha seli baada ya seli, seli baada ya seli, na kuziweka mbalimbali mezani, baada ya kila seli mwilini mwako, utafikia kwenye yai moja ndogo sana ambapo ulianzia, isiyoweza kuonekana kwa macho ya kawaida. Inakubidi kuangalia kwa darubini. Nimeona hiyo mbegu ya uhai chini ya darubini. Inaonekana kama kijiuzi kidogo sana. Na kitu cha kwanza kinachoanza ni moja kwa moja kwenye uti wa mgongo, ni kama kijifundo kidogo. Hiyo ndiyo seli ya kwanza ndogo inayolundikana juu ya seli.

⁴⁵ Sasa, kama ingenibidi kuchukua seli hiyo moja ambayo kila mmoja wenu alitokana, nayo seli moja ndogo sana, mbegu... Mbegu ni nini? Mbegu kitu kilicho kidogo sana, seli iliyo ndogo kuliko zote. Vema, ni nini kinachoifuata hiyo? Sasa, nimeumbua kila sehemu yako wewe, hadi kwenye seli hii moja ndogo, wala sijakupata bado. Nimezitandaza tu seli zako. Vema, basi, jambo linalofuata, seli za damu, na seli za nyama, na cho chote kile, ninaziweka zote hapa, lakini sijakupata bado. Na nimefikia mbegu moja sasa. Vema, nitaipangua seli hiyo ndogo. Sasa, uko wapi? Uhai wako. Na uhai ndio unaofanyiza seli ya kwanza, ambayo ni mbegu, kila kitu kwa asili yake; mbwa kwa jinsi ya mbwa, ndege kwa jinsi ya ndege, mwanadamu kwa jinsi ya mwanadamu. Kutengeneza seli, seli juu ya seli, seli juu ya seli, unafikia mahali ulipo, mwanadamu, ukitengeneza seli. Sasa, jambo hilo liliamriwa na Mungu kuwa hivyo.

⁴⁶ Lakini, sasa, na kansa je? Hebu na tuzungumze habari zake kidogo. Sasa, Mungu alikupa uhai wako. Na tuseme, wewe uko hapa leo, mimi hapa, hakuna—hakuna kitu mkononi mwangu, lakini huenda kukawa na kansa mkononi mwangu wakati mmoja. Vema, hiyo kansa ilifikaje hapo? Hebu tuone

kansa hiyo ni nini, sasa hebu na tumchambue, hebu twende tukamchukue. Sasa, yeye ni lundo la seli, pia. Mlipata kujua jambo hilo? Uvimbe, mtoto wa jicho, cho chote cha vitu hivyo ni seli. Hazina umbo. Nyingine husambaa, na nyingine zinafanana na buibui, na nyingine zinafanana... zinatoa milia, kansa nyekundu, kama tu nyuzi ndefu nyekundu ambazo zinaenea. Halafu kuna kansa ya rangi ya waridi jekundu ambayo kwa kawaida hutokea kwenye titi la mwanamke, ni kama mikate ya kumimina iliyolundikana, halafu inaenea. Nayo inakua kila mahali.

⁴⁷ Wakati mwingine vimbe hukaa mshazali, *hivi*, mrefu, mstatili, na kila namna. Hazina umbo, kwa sababu zinachukua umbo la pepo ambayo haina umbo. Lakini ni seli inayokua. Ni lundo la seli ambazo, tuseme, ndani yako sasa hivi kuna uvimbe ama kansa, inaunda seli, zinakua, zinakua, zinakua. Inakula, inafyonza uhai wako. Zinaishi kwa damu mwilini. Watoto wa jicho huchukua ute wa jicho na kumea moja kwa moja juu yake, wanajifunika, wanafunga macho yako. Baadhi yao huja wala hawafikii ninii... kwa mfano kinundu mwilini, ambacho huja katika virusi vidogo sana tu. Ukubwa wake haujalishi. Mbegu ya ukubwa ule ule humfanya ndovu, humfanya te—tekenya. Unaona? Ukubwa wa mbegu haujalishi.

⁴⁸ Na baadhi ya hizo hujitengenezea mwili, zingine hazifanyi hivyo kamwe. Na zingine haziwi seli. Zingine zinakuwa pepo, zipate kuitesa nafsi. Tutajaribu kufikia sehemu hiyo, nitaacha sehemu hiyo kwa ajili ya kesho alasiri, kama nikiweza, ambapo hayo mambo ya nafsi-roho yanavyokuja, na jinsi gani hushuka hapa *chini* hapa.

⁴⁹ Na sasa, marafiki, mimi sisimulii jambo hili kutokana na namna fulani ya saikolojia. Nimeshughulika na pepo kwa miaka mingi sana, nanyi mnajua jambo hilo. Laiti tu mngalijua jambo hilo, baada ya ibada kwisha usiku huu, ni nini kinachoendelea, wakati mwingine. Hamjui. Kumbukeni, unapomkabili pepo, afadhali ujue yale unayozungumzia. Usisimame tu hapo na kupiga makele, maana halitafaa kitu. Lakini hasa pepo analazimika kukutii, atatambua jambo hilo. Si vile unapiga makelele kwa nguvu, na si kiasi gani cha mafuta unachotia. Ni kile kilicho nyuma huku ndicho atakachotambua, ile Kweli. Yesu alimwambia tu, “Toka.”

⁵⁰ Kumbukeni, wale wanafunzi walikuwa wakipiga miguu kwa vishindo na kujinyonganyonga, na kujaribu kumtoa, na kila kitu. Wakasema, “Kwa nini hatukuweza kumtoa?”

Kasema, “Kwa sababu, ya kutokuamini kwenu.”

⁵¹ Kasema, “Mtoke.” Yule mvulana akaanguka na akawa na kifafa kibaya sana kuliko alichowahi kupata. Mnaona? Mnaona? Wao huyatambua mamlaka.

⁵² Angalia hao wavulana kule chini, hao wahuni waliomwona Paulo akitoa pepo. Walisema, “Tunaweza kufanya jambo lilo lilo,” watoto wa kasisi fulani. Kwa hiyo wakashuka wakaenda na kusema, “Tunaweza kutoa pepo.” Matendo 19. Wakashuka wakaenda kwa mtu aliyekuwa na kifafa, wakasema, “Tunawaapisha, kwa Yesu. Tokeni kwake!” Ibilisi akasema, sasa, “Katika Jina la Yesu ambaye Paulo anahubiri!”

⁵³ Huyo ibilisi akasema, “Sasa, Yesu namjua na Paulo namjua, lakini ninyi ni nani?” Mnajua kilichotukia. Akamrukia mtu huyo, na kurarua nguo zao, nao wakashikwa na kifafa wenyewe, na kukimbia kuingia mitaani.

⁵⁴ Pepo hao hao wanaishi leo, kwa hiyo kuna ushupavu mwingi wa dini. Hili ndilo kanisa, jioni ya leo. Kuna ushupavu mwingi sana wa dini nchini leo, unaoitwa uponyaji wa Kiungu, unapaswa kukomeshwa. Jambo hilo ndilo linaloleta fedheha kwa Huduma halisi. Hiyo ndiyo sababu mnapata shida sana. Kuna upuuzi mwingi sana unaoitwa dini, leo, huo unapaswa kukomeshwa; si kitu ila vikundi vilivyojitenga! Jambo hilo ndilo linalolifanya Kanisa la kweli la Mungu liwe na vita vikali na jambo hilo. Lakini sisi ni Wamarekani, unaona, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa. Mungu alisema ngano na mitambaazi na michongoma vilikua pamoja. Usijaribu kuving’oa. Viache vikue pamoja, lakini kwa matunda yao mtawatambua. Hakuna matunda, kwa nini, hakuna Uzima, hakuna kitu pale.

⁵⁵ Sasa, angalia seli hii. Hebu na tuseme, kwa mfano, kama vile mara nyingi, kansa nyekundu kwa kawaida huambukiza tumbo la uzazi la mwanamke, majeraha ya wanawake na kadhalika. Sasa huyo, hebu na tumchukue huyo, huyo jamaa sasa, kwenye seli yake, hii—hii kansa. Sasa kansa . . .

⁵⁶ Kila kitu katika maumbile ni mfano wa cha kiroho. Mnajua jambo hilo? Kila kitu katika maumbile ni mfano wa cha kiroho, haidhuru kiwe ni nini.

⁵⁷ Kwa mfano, kama hivi, wakati tunapozaliwa katika Mwili wa Kristo, kuna elementi tatu zinazohitajika kusababisha Kuzaliwa kwetu. Na hizo ni zile elementi tatu zilizotoka katika maisha ya Kristo wakati alipokufa. Kulitoka katika mwili Wake, maji, Damu, Roho. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Kweli.—”Mh.] Elementi tatu, hizo ndizo elementi tunazopitia tunapozaliwa mara ya pili: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa, hayo yote yanaweza kuwa katika tendo moja. Lakini inataka ninii . . . Lakini unaweza kuwa katika hali ya kuhesabiwa haki bila ya kutakaswa. Unaweza kumwamini Bwana Yesu Kristo na bado uendelee tu kuwa na uchafu wako. Lakini unaweza kuishi kabisa katika hali ya kuhesabiwa haki na kuishi maisha matakatifu pia, na bila kuwa na Roho Mtakatifu. Unaona, Biblia, Yohana wa Kwanza 5:7, ilisema, “Wako watatu washuhudiao Mbinguni, Baba, Mwana,

na Roho Mtakatifu... na Baba, Neno, na Roho Mtakatifu,” ambaye alikuwa ni Mwana, “na watatu hawa ni mmoja. Kisha wako watatu washuhudiaio duniani, maji, Damu, na Roho, nao hupatana kwa habari moja.” Si mmoja, lakini wanapatana kwa habari moja. Huwezi kuwa na Baba bila kuwa na Mwana; huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho Mtakatifu, kwa maana hawatenganiki, mmoja. Utatu uko katika mmoja.

⁵⁸ Sisikii jambo hilo hapa, lakini unalisikia sana kila mahali nchini, moja ya mambo makuu sana katika makundi ya Kipentekoste, ni kuchanganyikiwa katika jambo hilo moja rahisi. Nami nimekuwakutanisha viongozi wao pamoja na kuwathibitishia ya kwamba yote mawili yanaamini jambo lile lile. Ni Ibilisi kati yao, hivyo tu. Kama kanisa hilo kuu la Kipentekoste lingeu...lingetupilia mbali hayo mapokeo madogo ya kale, na kuungana pamoja katika Kanisa moja lililobarikiwa la Mungu, Kunyakuliwa kungekuja. Lakini mradi tu Shetani anaweza kuwashikilia wamegawanyikana, ni sawa. Hiyo ndiyo njia yake ya kufanya jambo hilo. Nao wanaamini jambo lile lile kabisa.

Mmoja anasema, “Vema, *hili* ni Lile”

⁵⁹ Nikasema, “Vema, kama *hili* ni Lile, basi Lile ni *hili*.” Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, yote ni mamoja. Lakini mambo ndiyo hayo, katika huo utatu wa utatu wa Mungu. Sasa, sasa, Mungu katika umoja Wake. Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Sasa, hatusemi “miungu yetu,” kama makafiri. Ni “Mungu wetu.” Unaona? Ni Utu wa Mungu wenye sehemu tatu.

⁶⁰ Sasa angalia, sasa, Shetani naye yuko kwenye utatu. Na nguvu zake ziko katika utatu.

⁶¹ Sasa, lakini angalia basi wakati maji, Damu na Roho vinaleta Uzao mpya. Hiyo ni kweli? Sasa angalia. Hilo ndilo linalowakilisha Kuzaliwa upya. Ni kitu gani kinachowakilisha kuzaliwa kwa kawaida kabla Kuzaliwa upya hakuja? Wakati...Ninyi akina mama, wakati mtoto mchanga anapozaliwa, kitu cha kwanza ni nini? Maji. Kinachofuata, damu. Kinachofuata, unaona, hiyo hufanyiza uzima, unaona, linamfanya mtu. Maji, damu, roho.

⁶² Sasa, kansa, hebu na tumshughulikie kama ninii yetu ifuatayo basi. Tuna kama dakika tano zilizosalia, nakisia. Kama dakika zingine tano, hebu na tushughulike na kansa. Jamaa huyo ni nini? Yeye anawakilisha nini? Yeye ni topasi. Anamwakilisha nderi, anakula vitu vilivyokufa. Na kansa inatokana na jeraha, mara nyingi, pale ambapo seli imeumizwa na ina—inavunjika. Na seli ndogo pale ndani inarudi nyuma. Loo, hilo ni neno kubwa kwa Wabatisti, sivyo? Vema, lakini inarudi nyuma, seli hiyo. Mimi ni Mbatisti ambaye anaamini katika kurudi nyuma.

⁶³ Mtu fulani alisema, hapa chini kwenye mkutano wa Arkansas juzi juzi, kasema, “Ndugu Branham,” kasema...

Alikuwa ni Mnazarayo mwenzangu. Alikuwa ameponywa. Alikuwa na ninii yake. . . Akitembea moja kwa moja mjini kote, akibeba mikongojo yake begani mwake. Akasema, “Unajua nini?” Kasema, “Nilipokuja hapa mara ya kwanza,” kasema, “Ni—nilifikiri wewe. . . nilikusikia ukihubiri, nilifikiri ulikuwa Mnazarayo.” Akasema, “Ndipo nikaona karibu watu wote walikuwa Wapentekoste, na mtu fulani aliniambia wewe ulikuwa ni Mpentekoste. Na sasa unasema wewe ni Mbatisti.” Kasema, “Sielewi.”

⁶⁴ Nikasema, “Loo, hilo ni rahisi.” Nikasema, “Mimi ni Mpentekoste Mnazarayo Mbatisti.” Kwa hiyo—hiyo ni kweli. Vema. La, sisi tu mmoja katika Kristo Yesu, kwa njia ya Roho Mtakatifu akitufanya mmoja. Hiyo ni kweli.

⁶⁵ Sasa, angalia, seli hii ndogo hurudi nyuma wakati inapojeruhiwa. Inaanza kidogo. Chembechembe zingine ndogo zinakimbilia mahali hapo zipate kutoa maisha yao. Na hivyo ndivyo usaha unavyoingia kwenye kidonda. Ni hivyo vijaskari vidogo sana vinavyopigania maisha yako. Vinakimbia kule na—na kuishambulia hiyo sumu, hizo nguvu za pepo zinazojaribu—zinazojaribu kukusanyika mle ndani, na kuyatoa maisha yao. Hilo ndilo linalosababisha. . . Hilo. . . Hao ni kundi la askari waliokufa, huo usaha ulio katika damu yako. . . ulio kwenye ki—kidonda, wanaoyatoa maisha yao wapate kuokoa yako.

⁶⁶ Sasa, mara seli ndogo inapokataana na hapo ndani ndipo huyu pepo anaanza, yeye huanza kukua, anaanza kuzidisha seli. Anaajenga mwili vile vile kama tu watoto wako wachanga wanavyoanza katika tumbo lako la uzazi, na kama ulivyoanza ndani ya mama yako. Seli juu ya seli, seli juu ya seli, seli, namna yo yote, mahali po pote; ninii tu, hawana umbo wa kitu cho chote kama mwanadamu, kwa jinsi yake. Zinatokana tu na roho fulani. Zinakua tu vyo vyote, na zitaanza seli juu ya seli, seli juu ya seli.

⁶⁷ Na sasa, muda si muda, utaanza kuwa mnyonge na kujisikia mgonjwa. Utamwendea daktari naye atakufanyia uchunguzi. Labda hawezi kuona. Kama akiipata, labda atakata. Kama anaweza kuikata aiondolee mbali, vema, umefanikiwa. Lakini kama hawezi kuikata aiondolee mbali, basi kama iko kwenye koo ama mahali fulani ambapo haiwezi kukatwa itoke, chembe moja ndogo yake itaendelea kuishi moja kwa moja. Unaona, kwa sababu si kama vile ungalikata mkono wako na kuuondolea mbali na itoshe, ama cho chote kile, ama kukatilia mbali. . . Ninalomaanisha, kama ungekata mwili wenyewe uuondoe, na kuuacha mkono wako mle, mbona, haungeweza kuishi. Lakini—lakini, unaona, hiyo haina aina ya uhai ulio nao. Ni nguvu za ibilisi zinazotenda kazi.

⁶⁸ Na sasa angalia, mnaiita, daktari anaiita, “kansa.” Mungu anaiita “ibilisi.” Angalia leo. Wao wanaipa tu. . . Neno *kansa* lilitoka wapi? Linatokana na. . . linatokana na neno la Kilatini

linalotumika katika lugha ya utabibu, linamaanisha “kaa,” kaa unayemwona pwani, aliye na miguu hiyo yote. Hivyo ndivyo hiyo—hiyo inavyofanya, inaenea, inasambaa. Neno kansa linamaanisha kaa. Nayo huingia na kuanza kujiimarisha na kufyonza damu inapoenea, kama vile pweza ama cho chote kile. Mbona, kivimbe, mtoto wa jicho, na magonjwa mengine, kila moja ya hayo hutokana na kirusi fulani, na kirusi hicho hakina budi kuwa mwili. Na kabla hakijakuwa mwili, hakina budi kuwa ni uhai fulani. Kabla hakijaweza kuumba ama—ama kupata uhai na kufanyiza seli zaidi, hakina budi kuwa ni uhai fulani. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, kansa hiyo ilitoka wapi? Nani, ilitoka wapi? Haikuwa ndani yako muda fulani hapa uliopita, lakini sasa labda imo ndani yako. Iilitoka wapi? Ni uhai tofauti na wako, unaoishi ndani yako. Nao unakutesa, unayafyonza maisha yako. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliuita “ibilisi.”

⁶⁹ Wao wanaita kifafa leo, wanasema, “kifafa.” Mbona, kifafa, katika Biblia, Yesu alikiita “ibilisi.” Wakati yule mtu alipokuja pamoja na yule mvulana aliyeanguka ardhini, na kutokwa na povu mdomoni, na kila kitu, yeye alisema, “Ana pepo, na mara kwa mara yeye humbwagwa motoni na majini.”

⁷⁰ Sasa wao walipamba jina lake na kumwita kifafa, lakini yeye ni pepo. Naye Yesu alisema, “Ewe pepo mtoke mtoto huyu!” Kweli kabisa. Sasa, kifafa kwa kawaida husababishwa na matatizo ya figo. Labda utajifunza jambo hilo baadaye kidogo. Mnaona? Yanasababisha kifafa, kutokana na ugonjwa wa mkojo.

⁷¹ Sasa, angalia kuhusu jambo hili, ndipo seli hiyo inakaa pale, ni pepo. Yeye anajenga uhai; anakua, anazidi kukua na kukua. Yeye ana jukumu moja la kufanya, hilo ni, kuutoa uhai wako. Hiyo ndiyo sababu ya kutumwa na Ibilisi, kupunguza siku zako chini ya miaka sabini.

⁷² Sasa, nampongeza kila daktari. Naam, bwana. Kila sayansi ya matibabu, Mungu na awabariki kwa msaada ambao wametoa kwa watu. Hiyo ni kweli. Ungefanyaje ulimwenguni leo bila hiyo? Ninamshukuru Mungu kwa sanyansi ya matibabu. Ninamshukuru Mungu kwa magari. Kama hakuwa amejalia sayansi kunitengenezea gari, ningekuwa na wakati mgumu nikija huku kwa miguu. Kwa taa za umeme, na kwa sabuni ya kunawa mikono yangu nayo, na dawa ya mswaki ya kusugulia meno yangu, hakika. Ninamshukuru kwa ajili ya kila kitu, kwa maana mambo yote mema hutoka kwa Mungu.

⁷³ Lakini hebu niwaambie, hakuna hata chembe moja ya dawa ambayo iliwahi kuponya magonjwa yo yote. Wala hakuna daktari hata mmoja, hakuna isipokuwa awe ni wa bandia, lakini daktari halisi atakwambia ya kwamba wao hawadai kuwa waponyaji. Papa hapa kwa Mayo Brothers,

wengi wenu... nimeshahojiwa kule, mara mbili ama tatu. Juu ya wagonjwa waliotoka kule, wasioweza kutibika... Mlisoma *Reader's Digest*, toleo la Novemba? Ni wangapi waliosoma toleo la Novemba, yale makala juu yangu humo ndani, kwenye *Reader's Digest*? Mnaona? Nao waliniita kule, yale mahojiano juu ya mtoto mchanga waliyekuwa wamemkatia tamaa. Kasema, "Jambo hilo halingewezekana." Lakini Roho Mtakatifu alinena nami na kuniambia jinsi lingefanyika, nalo likafanyika. Vema. Sasa, wao waliniita kule. Na papo hapo mlangoni ambapo Jimmy na hao wengine, Mayo walikuwa wanakaa pale, kuna ubao mkubwa sana uliosema, "Hatudai kuwa waponyaji. Tunadai tu kuyasaidia maumbile. Kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu." Hao ndio walio bora sana ulimwenguni. Sasa, tuna wachache walio wa bandia, ndio. Hiyo ni kweli. Tuna baadhi ya wahubiri wa bandia, pia. Vema. Kwa hiyo, jambo hilo linaendelea pande zote mbili.

⁷⁴ Angalia, lakini mtu ye yote anayedai kwamba ni mponyaji, yeye ni mwongo, maana hawezi kufanya jambo hilo. Kwa kuwa Biblia ilisema, "Mimi ndimi Bwana akusameheaye dhambi zako zote na kukuponya magonjwa yako yote."

⁷⁵ Nimekuwa nikisoma. Na chumbani mwangu, mle... baadhi ya madaktari walio bora sana nchini wamekuja kwangu. Hujui yaliyo nyuma ya maisha, ewe rafiki, kujua mambo ambayo yamekuwako, na mambo ambayo siyasemi hadharani. Watu huja kisiri. Na usikifikiri hakuna akina Nikodemo wengi bado ulimwenguni; hakika wako, maelfu yao. Wao wanaangalia jambo hilo na wanakuja mkutanoni. Wanaketi pale wamevaa T-shati, kitu fulani kama hicho, wenye majina maarufu sana hata ungalishangaa, wanaketi kabisa mkutanoni. Katika siku chache wanajificha na kuja kisiri, na kumtuma mtu fulani kwa mahojiano. Na kusema sasa hivi, wanasema, "Ndugu Branham, ninaamini Hiyo ni Kweli." Wao ni wanadamu kama tu tulivyo sisi. Hakika. Na kila mtu ana shauku ya kuangalia ng'ambo ya lile pazia jeusi huko ng'ambo anayopaswa kupitia siku moja.

⁷⁶ Lakini hizo kansa na mambo haya ni pepo kabisa waliojiundia mwili wa nyama, wakienea, wakiutoa uhai wako.

⁷⁷ Sasa, kama ningefanya kama daktari, kama ningeweza kuikata, kuiweka sakafuni... Ama, kama tu, tuseme, kwa mfano, wewe ungalikuwa kansa, wewe mwenyewe, hapa duniani. Sasa, huu hapa uponyaji wa Kiungu. Kama nilitaka kukuangamiza katika njia ya daktari, ningeweza tu... ingenibidi kusugua mwili wako, ama cho chote kile, mpaka utoweke duniani. Haungekuweko tena, kama tu vile daktari anavyoondoa kivimbe kutoka kwako. Lakini katika jinsi ya uponyaji wa Kiungu, kama wewe ungekuwa ni kansa, ningeuaita tu uhai wako ukutoke, nawe ungeaga dunia. Uhai wako ungekuacha, lakini mwili wako ungekuwa hapa kama tu vile ulivyokuwa.

⁷⁸ Sasa, hapo ndipo mahali ambapo kuona na wakati huwa ni adui mbaya sana wa Mungu katika uponyaji wa Kiungu. Sijui kama Ndugu Baxter anawahi kusikiliza mambo haya katika mikutano. Mimi huketi chini, ninamwelezea yeye pamoja na Ndugu Bosworth, ninarudia na kurudia. Lakini hivi ndivyo ilivyotendeka. Nina shaka kama wengi wenu enyi watu mnalipata, kwa sababu, baada ya kitambo kidogo, unaanza kuwaona watu wakirudi, wakisema, “Nilipata uponyaji wangu, Ndugu Branham, kwa siku mbili tatu, lakini, Mungu abarikiwe, u—umeniacha.” Nami naona jambo hilo, nami ninafikiri ni kwa sababu wao hawakai mkutanoni ipaswavyo. Watu hawaelewi. Nimewaona watu wakija jukwaani wakiwa vipofu kabisa, kansa, ama watoto wa jicho machoni mwao, na kusoma Biblia hii baada ya kuombewa, wanashuka kwenda zao; katika siku tatu ama nne wanakuwa vipofu tu kama walivyokuwa mara ya kwanza. Nini kimetukia? Mtu ye yote anajua ya kwamba wakati uhai unapoondoka katika mwili wo wote, unasinyaa kwa kitambo kidogo. Hiyo ni kweli?

⁷⁹ Kuna mtu aliyewahi, hapa, kuua kulungu, ama ng’ombe, ama kitu kama hicho? Hakika. Vema. Unampima usiku wa leo, ninyi wawindaji huku, marafiki zangu. Unamwua kulungu na kumtupa kwenye mizani, unawaambia vijana ana uzito gani. Angalia! Asubuhi atakuwa amepungua ratili kadha kuliko alivyokuwa. Wakati mwanadamu anapokufa, mzishi, jambo la kwanza, anaondoa meno ya bandia ama jicho la bandia, cho chote kile kule ndani, anakitoa; kwa sababu, husinyaa, vitatokeza kwa sababu mwili wa mwanadamu hupungua. Mwili mwingine wo wote husinyaa. Wakati uhai unapotoka kwenye seli, unaanza kushuka, kupungua. Utafanya hivyo kwa kama masaa sabini na mawili. Na ndipo utaanza kuvimba. Hebu mbwa mdogo na akanyagwe, huko nje barabarani. Hebu na alale pale kwenye jua kwa muda wa siku tatu hivi, na uone kitakachotukia. Yeye ni mbwana mkubwa kuliko alivyowahi kuwa. Anavimba. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁸⁰ Vema, hilo ndilo jambo lile lile linalotukia wakati pe—pepo anapotolewa kutoka kwa mgonjwa. Siku chache za kwanza, “Loo, ninajisikia vizuri sana.” Kisha anaanza kusema, “Mimi—mimi ni mgonjwa kuliko—kuliko nilivyowahi kuwa. Nimepoteza uponyaji wangu.” Hakika tu kama vile imani ilivyomwondoa, kutokuamini kutamrudisha moja kwa moja tena. Kama vile imani inavyoua kitu hicho, kutokuamini kunakifufua. Yesu alisema, “Pepo mchafu anapomtoka mtu, hupitia katika mahali pakavu kisha anarudi pamoja na pepo wengine saba. Na kama yule mtu mwema mwenye nyumba hasimami pale kuulinda mlango, yeye atakuja aingie moja kwa moja. Na mwenye nyumba yako ni imani yako. Sema, “Nenda zako!” Hivyo ndivyo ilivyo.

⁸¹ Lakini sasa mwangalie mgonjwa aliyeponywa, kwa kawaida, isipokuwa iwe ni muujiza mkubwa sana. Ambapo, kuponya

Kiungu na muujiza ni mambo mawili mbalimbali. Kuponya Kiungu, jambo moja; muujiza ni jambo lingine. Lakini uponyaji wa kawaida wa Kiungu, wakati pepo mchafu anapotolewa, pepo wa kansa, wakati anapomwacha mtu, “Loo!” Sasa, ama tuseme tutachukua jambo fulani ili uweze kuona vizuri sana, nitasema, mtoto wa jicho. Nini kilitendeka wakati yule mtu... Kama ukimwangukia kipofu. Sijui kama nimeisha wahi kuwa na mmoja hapa ama sijakuwa naye, bado, macho yenye watoto wa jicho. Nitawaacha wasimame kwa dakika chache. Kwa nini? Ili kwamba kule kusinyaa kuanze kutukia. Ninawaambia warudi, watupe ushuhuda. “Loo, jamani!” Wanaweza kuona vizuri sana. “Loo, jamani! Ninii tu, ninaweza kuona vitu! Naam! Mimi...” Kuna nini? Uhai umeondoka; mwili wa mtoto wa jicho unasinyaa. Vema, utafanya hivyo kwa siku kadha. Anasema, “Loo, ninaendelea vizuri sana.”

⁸² Na baada ya kitambo kidogo, wanaanza kuumwa na kichwa, hawajisikii vizuri sana. Wanaamka kesho yake, “Ninaanza kuwa kipofu tena.”

⁸³ Baadhi yao walisema, “A-ha, ulichochewa tu. Kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha lilikuchochewa tu.” Usiamini uongo huo! Huo ni uongo wa Ibilisi. Kama ukiuamini, utakuwa kipofu tena moja kwa moja.

Lakini kama utashikilia tu, useme, “La. Bwana, ninaamini.”

⁸⁴ Basi nini kinatukia? Mwili huo unavimba kwa muda fulani. Unaziba tena hilo jicho. Hiyo kansa mwilini itavimba. Utaanza kuumwa na kusikia uchungu tena. Halafu utakuwa mgonjwa sana, mgonjwa vya kutisha. Kwa nini? Uvimbe mkubwa wa nyama zilizokufa ndani yako umekaa pale, umekufa.

⁸⁵ Unarudi, kwa daktari naye anasema, “Loo, huo ni upuuzi. Hiyo papo hapo. Naweza kuiona.” Hakika, ipo, ila imekufa. Haleluya!

⁸⁶ Sasa, mzunguko wa damu mwilini hauna budi kuusafisha mwili. Kila wakati moyo unapopiga, unaitupa damu kuzunguka mwilini, nayo inaokota usaha huo. Hakika, linakufanya uwe mgonjwa. Vipi kama ungekuwa na kipande cha nyama kinachoning’inia mahali fulani ndani yako, ama kirefu kama nyoka, ama kitu chenye ukubwa kama wa kidole chako, na kinaning’inia mle ndani, na kimekufa, kiasi hicho cha nyama iliyokufa ikining’inia ndani yako, na inaoza? Vema, bila shaka, damu mwilini mwako haina budi kukisafisha hicho, inapopitia mle. Lakini kuna mwili uliokufa, kitu hicho kinachoning’inia pale, kwa sababu uhai umetoka mle ndani. Nguvu za Mungu, kupitia katika imani, ziliuondoa. Yeye ni pepo; hana budi kuondoka.

⁸⁷ Lakini, sababu yake, watu hawajafunzwa. Wanakwenda zao, wanakata tamaa. Na pepo yuyo huyo amesimama pale pale, ili achukue mamlaka tena. Mungu anapokwambia cho

chote kwenye jukwaa hili, kwa Roho Wake, chini ya upako, usitilie shaka jambo hilo, ama jambo baya zaidi litakupata, Yeye alisema. Kwa kuwa Yesu alisema, “Hali ya mwisho ya mtu huyo ilikuwa ni mbaya mara saba kuliko ilivyokuwa hapo kwanza.” Hiyo ni kweli? Wakati pepo mchafu alipomtoka mtu, alitembea katika mahali pakavu, akarudi pamoja na pepo wengine saba. Kwa hiyo, usiache kuamini. Lishikilie moja. Maanisha hilo moyoni mwako. Useme, “La, bwana! sitatikiswa! Haidhuru nitakuwa mgonjwa jinsi gani, hilo halina uhusiano wo wote nalo.” Halafu, muda si muda, utakuwa unapata afya. Kila kitu kitakuwa sawa basi. Unaona, imekufa. Ule—ule upasuaji ambao daktari angeitoa toka kwako, uvimbe uo huo umo ndani yako, bila uhai ndani yake.

⁸⁸ Unasema, “Uhai ulio ndani yake, Ndugu Branham, utaniondolea uhai wangu?” La, bwana. Uhai huo ni uhai tofauti na wako. Nimekuonyesha hivi sasa tu ya kwamba wewe ni uhai na unakuwa mtu, yenyewe ni uhai na inakua kitu chenye uhai; nawe ni wa Mungu, na yeye ni wa Ibilisi. Mnaona ninalomaanisha? Elimu juu ya pepo. Sasa, unapaswa kuona kitu hicho kinavyoonekana unaposimama na kukiangalia.

⁸⁹ Loo, jamani, ninasikitika, inakaribia saa tisa na nusu. Samahani. Angalieni, marafiki. Loo, kile ulimwengu huu unachohitaji!

⁹⁰ Nimekuwa humu karibu miaka saba, nikifundisha kila mahali Marekani, nikiwa na ibada hizi za uponyaji. Nimepata wazo jema nianze kuzunguka tena nchini, kufundisha Biblia, na juu ya elimu juu ya pepo, jinsi watu wanavyoweza kufahamu la kufanya. Na hiyo ndiyo sababu, wao wanahudhuria mikutano hii, mara nyingi, na, jamaa... Kama hufahamu, hao watu wanatoka na mara nyingi...

Sasa, mnakumbuka yule jamaa aliyekuwa na kusema alikuwa na kipawa cha uponyaji wa Kiungu? Kipawa cha kuponya Kiungu kilikuwa ndani yako kama uliponywa. Ni wewe, wewe ndiye. Kipawa cho chote hutenda kazi kwa imani. Na haidhuru nina kipawa kiasi gani cha uponyaji wa Kiungu, ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote, lakini ungaliweza kusimama hapa na, kama huna imani ya namna ile ile, haitakufaa kitu. Ningeweza kukuombea, kwa masaa kadha na majuma kadhaa na miezi. Si wahubiri walio na uponyaji wa Kiungu. Wewe ndiwe uliye na uponyaji wa Kiungu, unayeamini katika kuponywa, maana ni kwa imani. Kwa imani! Kila kazi ya Mungu ni kwa imani.

⁹¹ Silaha zote za Mungu ni kwa imani. Hatuna kitu hata kimoja chenye asili ya ulimwengu huu. Kila kitu cha kanisa la Ki—Kikristo ni tendo la imani. Zianganilie silaha za Mungu, upendo, furaha, amani, saburi, wema, upole, utu wema, uvumilivu. Hiyo ni kweli? Kila kitu ni cha kimbinguni, hakuna cha

kawaida. Kwa hiyo hatuungalii mambo ya kawaida, kwa sababu tunatenda kazi kimbinguni. Na jinsi tu tunavyoweza kuliwekea msingi, ni imani, ndiyo Mungu alisema ilikuwa Kweli, nasi tunaangalia Yasiyoonekana. Nasi tunaita hayo mambo ambayo hayapo, kana kwamba yapo; kama vile alivyofanya Ibrahimu, naye akalipata jambo hilo. Amina! Ibrahimu aliviita vitu hivyo ambavyo havikuwepo, kama Mungu alivyofanya, kama kwamba vilikuwepo. Akiwa na umri wa miaka mia moja, hakusitasita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini.

⁹² Ningeweza tu kuwazia jambo hilo, nawe je? Ninamwona Sara akiamka asubuhi moja. Mungu akasema, "Ibrahimu!" Kasema, "Ibrahimu, utapata mtoto."

⁹³ Sara akaamka. Kasema, "Unajisikiaje, Sara?" Hili ni kundi lililochanganyikana, lakini sikilizeni.

"Hamna tofauti."

⁹⁴ "Vema, Mungu atukuzwe, tutampata! Nenda katafute vijiatu vya mtoto na pini, na kila kitu. Jiandae."

Vema, mwezi mwingine ukapita. "Sara, unajisikiaje?"

"Hamna tofauti."

Mwaka ukapita. "Sara, vipi sasa?"

"Hamna tofauti."

Miaka kumi ikapita. "Sioni tofauti."

Mika ishirini na mitano ikapita. "Hamna tofauti."

⁹⁵ Ibrahimu, badala ya kuwa mnyonge, alipata na nguvu zaidi na zaidi. Alijua wakati wote itakuwa ni muujiza zaidi wakati wote, maana yeye alimwanimi Mungu, naye hakusitasita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini. Alisema, "Tutampata!" Na asubuhi moja tumbo la uzazi la Sara likaanza kuvimba, na mtoto Isaka akazaliwa, kwa maana Ibrahimu alimwanimi Mungu. Naye aliyaangalia mambo hayo, na kuyahesabu mambo hayo yasiyokuwepo kana kwamba yalikuwepo.

⁹⁶ Si kwa kujisikia, si kwa kuona. Huishi kwa kujisikia wala kwa kuona. Ni kwa imani. Na wakati Mungu ameahidi jambo lo lote, kasema, "Yo yote muombayo, aminini mtapokea," kisha shikilieni jambo hilo. Mungu alisema hivyo, halina budi kutimia! Amina. Pepo!

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, watatu katika
Mmoja;
Pepo watatetemeka na wenye dhambi
wataamka;
Imani katika Yehova itatetemesha cho chote
kile.

Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Bila shaka ndivyo ilivyo. Iweni na imani katika Mungu. Mtazameni Yeye. Msisogee. Kaeni papo hapo. Ndivyo Mungu alivyosema!

⁹⁷ Na, pepo, ni nini? Hao ni viumbe vya kiroho. Sasa, da—daktari anasema, “Una kansa. Una TB. Una mtoto wa jicho. Una kikomi. Una *hiki*.” Ni pepo. Ni uhai, na nyuma ya uhai huo ni roho. Ni wangapi wanaojua na wanaweza kuona kwamba kansa, mtoto wa jicho, vina—vina— . . . Ni roho, lakini, ama vina—vina uhai ndani yake. Vema, hakuna kinachoweza kuwa na uhai bila roho, mnaona, kwa hiyo hapana budi pawe na uhai unaoendeleza kitu hicho, mahali fulani.

⁹⁸ Hata ule mti pale una uhai ndani yake. Sayansi yote ulimwenguni haiwezi kutengeneza unyasi mmoja. Mlipata kujua jambo hilo? Wanatengeneza kitu kinachofanana nao, lakini hawawezi kupata fomula ya uhai. Hiyo ni Mungu. Mnaona? Yesu aliuambia ule mti, “Ulaaniwe. Huna tunda lo lote, wala hutazaa lo lote.” Wakapita kule nyuma kabisa. Ilikuwa yapata saa mbili asubuhi hiyo. Wakapita kama saa tano, walipokuwa wanaenda kula chakula cha kutwa. Petro akasema, “Angalia ule mti, umekufa kutoka mizizini kwenda juu.” Kwa nini? Yesu aliukemea ule uhai uliokuwemo katika ule mti, uliokuwa kwenye mizizi, na kitu hicho chote kikafa. Haleluya!

⁹⁹ Kristo yuyo huyo anaweza kukemea kansa kutoka kwenye mizizi, na kitu hicho chote kitakufa. Mti huo ulikuwa umesimama pale kama tu ulivyokuwa, masaa kadha hapo awali, lakini unaona majani yakianza kupukutika, halafu unaona maganda yanaanza kutoka. Na ninii . . . Ukaanza kukauka, siku baada ya siku, juma baada ya juma, na baada ya muda kidogo hapakusalia hata na chembe ya mti huo. Haleluya! Kansa, uvimbe, mtoto wa jicho, ama cho chote kile, itakibidi kuondoka wakati Kristo anaponena. Yeye alitoa pepo. Naye akasema, “Kwa Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka, ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikonzo yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

¹⁰⁰ Mnampenda? Ninasikitika niliwaweka saa nzima hapa alasiri ya leo, mmekeiti hapa. Mnampenda Bwana? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni jambo gani litakalotukia sasa? Kama ukimkubali Kristo kama mponya wako, na uamini moyoni mwako ya kwamba jambo fulani limetukia kwako . . . Na uamini ya kwamba umeponywa? Utaamini ya kwamba umeponywa? Usimwache Ibilisi akubandike jambo lo lote lingine. Wewe endelea tu.

“Daktari,” kasema—kasema, “daktari, inaonekanaje?”

Akasema, “Mbona, bado ingalipo.”

¹⁰¹ Moyoni mwako unajua, unajua jambo lililotukia. A-ha! Muda si muda, wasema, “Hivi, Kile kitu kimekwenda wapi?”

¹⁰² Ndipo useme, “Angalia, daktari, nitakwambia. Hivi ndivyo ilivyotendeka, Yesu Kristo aliniponya. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo aliniponya.”

¹⁰³ Vema, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Ndugu Willett, waweza kuja kwa muda kidogo tu, ndugu?

¹⁰⁴ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya Damu ya Kristo. Na labda wakati mwingine kwamba mtumishi Wako, Bwana, hatumii hekima, kwa kuzungumza kwa muda mrefu. Lakini labda naweza kujisikia kama Paulo, aliyehubiri usiku kucha usiku mmoja. Maskini jamaa mdogo akaanguka kutoka dirishani na akafa. Naye mtume huyo, akiwa na Neno la Mungu maishani mwake, aliondoka akaenda akaweka mwili wake juu ya mvulana huyo, uhai ukaingia ndani yake naye akaishi tena.

¹⁰⁵ Mungu mpendwa, ninatambua ya kwamba jua la ustaarabu huu mkuu linatua, saa imepita sana, mchana umekwisha, vivuli vya jioni vinashuka. Mwanga Mkuu unatokea kutoka katika Ufalme wa Mungu, kuchukua mahali pa giza hili kuu linalokuja juu ya nchi. Mungu, ninatambua ninazidi kuwa mzee kila siku. Nijalie niende, Bwana. Nipe nguvu. Nisaidie kutangaza Kweli hii kuu kila mahali. Tusaidie, kesho alasiri, ili tupate kufahamu zaidi.

¹⁰⁶ Na, Mungu mpendwa, wabariki wasikilizaji hawa wachache alasiri ya leo. Usiku huu, watakapokusanyika kwa ajili ya ibada ya uponyaji, naomba kila mtu na kila mwanamke amwendee mwingine na waaze kuzungumza, na kusema, “Sasa, hapa kuna . . . usi—sitilie shaka tena. Tunafahamu mahali linapotoka sasa. Tunajua ni ibilisi. Nasi tunajua atakapoondoka, hana budi kuja kwa amri ya Mungu. Ni lazima aje. Mungu tayari amesema jambo hilo. Hana budi kuondoka.” Halafu, naomba waondoke, wakiwa na furaha, wakishangilia, wakidai uponyaji wao. Hakuna jambo, jalia kusiweko na jambo lo lote litakalowazuia, tena; waende tu, wakiadini.

¹⁰⁷ Na, Mungu, jalia kanisa hili dogo hapa, na makanisa haya yanayoshirikiana hapa, yawe na ufufuo baada ya mkutano huu, Bwana, utakaowajaza tele na mamia ya watu waletwe kwenye Ufalme wa Mungu. Tujalie, Baba. Naomba wanaume na wanawake wengi hapa, kutoka kila mahali nchini na mahali pengine, naomba waupeleke Ujumbe kwa makanisa yao, nao naomba wapate ufufuo wa mtindo wa kale. Tujalie hayo, Bwana. Tusamehe dhambi zetu sasa. Tusaidie kuwa watumishi Wako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁰⁸ Sijui, wakati mnapoketi hapa, je, kuna mwenye dhambi ye yote humu jengoni leo, angesema, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi”? Je, utainua mkono wako? Kuna mwenye dhambi? Sininii. . . Mungu akubariki, mama. Yuko? Mungu akubariki, bwana. Nawe, na wewe, na wewe, Mungu awabariki. Sijui kama . . . Sasa, hili ni kwa ajili yenu.

¹⁰⁹ Mnaona, siamini katika kurudi kwa wasikilizaji. Siwalaumu wale wanaofanya jambo hilo. Siamini katika kuingia kati ya wasikilizaji na kujaribu kumvuta mtu fulani. Unaona? “Hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu.” Mnaona? Hiyo ni kweli. Unamvuta tu kumpeleka pale kinyume cha mapenzi yake. Unaona? Lakini kama Mungu akibisha moyoni mwako, wewe ni mtu aliyejaliwa sana ulimwenguni. Hamjui tu ni watu wangapi ambao nimesema nao.



Elimu Juu ya Pepo — Milki ya Kimwili

8 Juni, 1953, Jumatatu alasiri

Roberts Park Amphitheater, Connersville, Indiana

Elimu Juu ya Pepo — Milki ya Kidini

9 Juni, 1953, Jumanne alasiri

Roberts Park Amphitheater, Connersville, Indiana

Roho Zinazoshawishi

24 Julai, 1955, Jumapili asubuhi

Maskani Ya Branham, Jeffersonville, Indiana

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham, zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza, zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org